

# CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE



## MAHAFALI YA KUMI NA NANE (18) KAMPASI YA KIVUKONI, MAHAFALI YA NANE (8) KAMPASI YA KARUME ZANZIBAR NA MAHAFALI YA KWANZA (1) KAMPASI YA PEMBA- 2023

Mkuu wa Chuo anawatangazia wanafunzi waliohitimu masomo yao katika mwaka wa masomo 2022/2023 kwamba **Mahafali ya Kumi na NANE** yatafanyika kwenye Kampasi ya Kivukoni, siku ya **Ijumaa tarehe 24 Novemba, 2023** kuanzia saa **TATU ASUBUHI, Mahafali ya NANE** katika Kampasi ya Karume Zanzibar yatafanyika siku ya **Jumatatu tarehe 27 Novemba, 2023** na Mahafali ya **KWANZA** Kampasi ya **PEMBA** yatafanyika siku ya **Jumatano, tarehe 29 Novemba, 2023**.

### WAHITIMU WANATAKIWA KUZINGATIA YAFUATAYO:

- 1 kwa Wahitimu wa **Kampasi ya KIVUKONI** wanatakiwa kuchukua Majoho kwenye ofisi namba 115 – Jengo la Uhuru Kampasi ya **Kivukoni** kuanzia **Ijumaa, Tarehe 17 siku ya Ijumaa** hadi **Alhamisi, tarehe 23 Novemba, 2023** wakati wa saa za kazi. Kwa Kampasi ya **Karume - Zanzibar** wafike Ofisi ya PMU kuanzia **Tarehe 25 hadi Jumapili Tarehe 26 Novemba, 2023** kuanzia saa **4:00 asubuhi hadi saa 9:00 Alasiri**. Na Kwa Kampasi ya **PEMBA** Majoho yatatolewa Tarehe **27 na 28 Novemba** katika ofisi za PMU na zoezi la namna ya kupokea vyeti litafanyika Chuoni **PUJIN** Tarehe 28 saa **NANE Mchana. MAJOHO HAYATATOLEWA SIKU YA MAHAFALI.**
2. **MALIPO YA MAJOHO NI SHILINGI AROBAINI ELFU NA MALIPO YOTE YAFANYIKE KWA KUTUMIA CONTROL NAMBA.**
3. Majoho sharti yarejeshwe Chuoni kabla ya **tarehe 3 Desemba, 2023** kwa **Kampasi ya Kivukoni na Kampasi ya Karume- Zanzibar**. Vinginevyo **faini ya shilingi 10,000/=** itatozwa kwa siku kwa yeyote atakayechelewa kurudisha joho hilo. Pia kwa yeyote atakayepoteza atawajibika kulipia.
4. Zoezi la namna ya kupokea vyeti (**rehearsal**) litafanyika **Alhamis, tarehe 23 Novemba, 2023** kuanzia saa **6.00 mchana** katika uwanja wa Mahafali **Kampasi ya Kivukoni** na kwa **Kampasi ya Karume-Zanzibar** zoezi hilo litafanyika **Jumapili tarehe 26 Novemba, 2023** kuanzia saa **4:00 asubuhi** katika uwanja wa mahafali. **Mhitimu atakayeshindwa kuhudhuria zoezi hilo, hataruhusiwa kushiriki katika Mahafali hayo.**
5. Kila Mhitimu atapaswa kujigharamia Usafiri, Malazi na Chakula.
6. Kusanyiko la wahitimu wote (**CONVOCATION**) waliosoma katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere litafanyika **Alhamis, tarehe 23 Novemba 2023** katika Ukumbi mpya wa Mihadhara, (**NEW LT**) Prof. **COLIN LEYS** chuoni hapo kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa sita mchana.

7. Washiriki wote wa Mahafali wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao kwa **kupiga simu namba 0782405552/ 0765016710 AU 0620508571**

Nyote Mnakaribishwa.

Mkuu wa Chuo,  
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,  
S.L.P. 9193,

**DAR ES SALAAM.**

Simu: +255 22 2820041/ 2820045/ 2820047

Faksi: +255 22 2820816

Barua pepe: [rector@mnma.ac.tz](mailto:rector@mnma.ac.tz)